TAARIFA YA UTEKELEZAJI MRADI MALIPO KWA UFANISI (RBF) MKOA WA MWANZA

KWA MHE. MKUU WA MKOA WA MWANZA

Mpango wa malipo kwa ufanisi (Result based financing) ni mradi unaofadhiliwa na Bank ya dunia kwa serikali ya Tanzania wenye lengo la kuboresha afya msingi (To improve primary health care). Mradi huu ulianza kutekelezwa mkoa wa Shinyanga mwaka 2015.

Mkoa wa Mwanza ulianza kutekeleza Mpango wa malipo kwa ufanisi (RBF) mwezi wa nne 2016 ikiwa ni Mkoa wa pili kutekeleza mradi huu baada ya Shinyanga. Mradi huu ulianza mwaka mmoja uliyopita baada ya vituo vyote vya kutolea huduma za afya mkoa wa mwanza kufanyiwa BRN star rating na matokeo yalionyesha kuwa 40% (153) vilipata nyota moja mpaka tatu kati ya vituo vyote vya Mkoa wa Mwanza ambavyo ni 384.Matokeo ya BRN star rating yalikuwa kama ifuatavyo, kituo kimoja kilipata nyota 3, vituo 5 vilipata nyota 2 na vituo 147 vilipata nyota 1. vituo vya umma ni 252 kati vyote 384 ambavyo ni sawa na 65%, hivyo basi vituo vya umma ambavyo vipo kwenye mpango wa malipo kwa ufanisi ni 153 kati ya 252 sawa 60%.

Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, jinsia, wazee na watoto ikishirikiana na ofisi ya Rais TAMISEMI iliandaa viashiria vya utoaji wa huduma katika ngazi ya zahanati, vituo vya afya na hospitali zote ngazi ya halmashauri. pia waliaandaa viashiria vinavyotakiwa kufikiwa na timu za usimamizi ngazi ya halmashauri(CHMTs) na mikoa (RHMT). Viashiria hivi vitapimwa kila robo mwaka na ndivyo vimekuwa msingi wa malipo kwa ufanisi. Zahanati ikifikia viashiria vyote italipwa mil.5, kituo cha afya kitalipwa mil.25 na hospitali italipwa mil.71.

Mpango wa malipo kwa ufanisi unahusisha vituo vyote vya umma vilivyopata nyota 1 na kuendelea, pamoja na vituo vya mashirika ya dini (Faith Based Organization) yaliyoingia makubaliano ya utoaji huduma za afya na halmashauri husika, ikiwa ni pamoja na kutoa huduma bila malipo kwa makundi maalum yaliyotambuliwa na sekta ya afya ya mwaka 2007 kama watoto chini ya miaka 5, wazee wenye umri zaidi ya miaka 60 nk.

Pia timu za usimamizi huduma za afya ngazi ya halmashauri (CHMTs) zote 8 mkoa wa mwanza Pamoja na timu ya usimamizi huduma za afya ngazi ya mkoa (RHMT) zimejumuishwa kwenye mpango wa malipo kwa ufanisi (RBF).

Kabla ya kuanza mpango wa malipo kwa ufanisi vituo vyote vya kutolea huduma kasoro hospitali zote vilipewa fedha kiasi cha Tshs 10,000,000/= kama" start up fund" ili kuboresha miundo mbinu ya kutolea huduma za afya, hadi sasa vituo vyote vimekwisha tumia fedha hizo na kuboresha miundo mbinu kwa kiasi kikubwa . wakati wa utelezaji wa shughuli hii kulijitokeza changamoto kama matumizi mabaya ya fedha za umma , kufanya manunuzi bila kufuata sheria ya manunuzi, kutoweka kumbukumbu za fedha kama cashbook, payment vocha, cheque book, EFD risiti, kutoshirikisha watallamu husika toka halmashauri husika n.k,

Malipo yaliyofanyika ngazi zote mkoa wa Mwanza kwa robo zote(Apr-Jun, Jul-Sept, Oct-Dec 2016)

Name of Entity	**Amount in Tshs. April-June**	**Amount in Tshs. July-Sept 2016**	**Amount in Tshs. October-December 2016**
Administrative Entitie(CHMTs)	125,296,433	145,504,220	172,893,961
Hospitals	347,348,207	412,475,996	413,928,982
Council's HFs(HCs & Dispensaries)	131,992,587	206,305,324	240,917,245
RHMT	12,431,733	10,041,015.16	22,149,298
RS (Verification Fund)	73,478,230	66,521,739	66,521,739
Grand Total Region	**690,547,190**	**840,848,294**	**916,411,225**

Mwenendo wa malipo robo zote (Apr-Jun, Jul-Sept, Oct-Dec 2016)



	Administrative Entitie(CHMTs)	Hospitals	Council's HFs(HCs & Dispensaries)	RHMT Entity	RS Entity
April-June	125,296,433	347,348,207	131,992,587	12,431,733	73,478,230
July-Sept 2016	222,066,974	412,475,996	206,305,324	10,041,015.16	66,521,739
October-December 2016	172,893,961	413,928,982	240,917,245	22,149,298	66,521,739

MAELEZO: kutokana mchoro huu, Malipo ktk ngazi ya CHMTs VItuo vya afya na zahanati yameongezeka ikilinganishwa na Hospitali na RHMT.

Mwenendo wa malipo yalifanyika kwa vituo vya afya kwa robo 2(Jul-Sept 2016 & Oct-Dec 2016)



MAELEZO: kutokana mchoro huu, Malipo ktk ngazi ya VItuo vya afya kwa baadhi ya vituo yameongezeka kwa robo ya oct-des 2016 ikilinganishwa na july-sept 2016

Fedha zilizotengwa ukilinganisha na fedha zililizolipwa mkoa wa Mwanza, Oct-Dec 2016



MAELEZO: Mchoro huu, Unaonyesha Malipo yaliyolipwa ukilinganishwa na fedha iliyotengwa.

Mwenendo wa malipo yalifanyika kwa CHMTs kwa robo 2(Jul-Sept 2016 & Oct-Dec 2016)



MAELEZO: kutokana na mchoro huu, Malipo kwa baadhi ya CHMTs yameongezeka

Mwenendo wa malipo yalifanyika kwa Hospitali kwa robo 2(Jul-Sept 2016 & Oct-Dec 2016)



	Magu Hospital	Sumve DD Hospital	Sengerema DD Hospital	Ngudu Hospital	Bukumbi Hospital	Misungwi Hospital	Nyamagana Hospital
July-Sept 2016	65,650,903	67,481,805	59,635,083	48,649,673	58,065,739	50,219,017	62,773,772
October-December 2016	53,880,821	68,266,477	63,558,444	51,265,247	61,088,070	58,065,739	57,804,182

MAELEZO: kutokana mchoro huu, Malipo ktk ngazi ya hospitali yameongezeka kwa baadhi na zingine kupungua.

CHANGAMOTO:

- Halmashauri kutohusisha wataalamu wengine tofauti na afya wakati wa utelelezaji wa RBF
- ukosefu wa vitabu vya kutunza ku bukumbu za mapato na matumizi ya fedha zilizotumwa (mil. 10)
- ukosefu wa vitabu vya kupokelea na kutolea mali zinazonunuliwa kwa fedha za RBF
- Udhaifu wa utunzaji wa nyaraka za utekelezaji wa mpango wa RBF
- Uelewa mdogo wa watumishi kuhusu taratibu za usimamizi wa fedha za serikali.

Naomba kuwasilisha

Dr. SILAS WAMBURA

KAIMU MGANGA MKUU (M)

MWANZA